

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS IKULU**

Simu: 255-262961500/1
Nukushi: 255-262961502
Barua pepe : press@ikulu.go.tz
Tovuti : www.ikulu.go.tz



OFISI YA RAIS,
IKULU,
1 BARABARA YA JULIUS NYERERE,
CHAMWINO,
S.L.P 1102,
40400 DODOMA.

Seoul
04 Juni, 2024

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan amesema ana imani mkutano wa Korea na Afrika utafungua milango ya ushirikiano wa kiuchumi na teknolojia kwa faida ya maendeleo ya Afrika.

Rais Samia ameyasema hayo katika mkutano wa Korea na Afrika unaofanyika Jamhuri ya Korea kwa lengo la kujenga ushirikiano wa nchi hiyo na Bara la Afrika.

Pia Rais Samia amesema kuna fursa ya kipekee katika kuunda ushirikiano wenye malengo mahsusi ya kiuchumi ili kutafuta ufumbuzi wa tofauti za maendeleo ya kijamii na kiuchumi katika nchi za Afrika.

Kwa kuzingatia hayo Rais Samia anatarajia nia thabiti ya Korea katika mafanikio ya pamoja na kuunga mkono kuundwa kwa mpango kazi wa kushirikiana kwenye biashara na uwekezaji bila kuisahau sekta binafsi.

Pamoja na kampuni moja ya Korea kushirikiana na Tanzania kwenye masuala ya madini ya kinywe, Rais Samia amewakaribisha wengine nchini kwa ajili ya ushirikiano zaidi kwenye uchimbaji na utafiti wa madini ya kimkakati.

Vile vile, Rais Samia kama kinara wa masuala ya nishati safi barani Afrika ambayo itawasaidia sana wanawake amesisitiza umuhimu wa kuwekeza kwenye nishati hiyo si tu kwa ajili ya kupunguza hewa chafu ila pia kupunguza uharibifu wa mazingira.

Wakati huo huo, Rais Samia alikutana na kufanya mazungumzo na Rais wa Shirika la Korea (KOICA) Bw. Chang Won Sam ambapo wamezungumzia namna ya kuendeleza ushirikiano wa miradi mbalimbali.

KOICA hadi sasa inatekeleza miradi 10 katika sekta za maji, afya na elimu ikiwemo kuimarisha afya ya mama na mtoto, kuanzisha huduma za usambazaji maji kwa maeneo ya mijini na vijijini ikiwemo Dodoma na Arusha.

Rais Samia anatarajia kuendela kushiriki katika Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali kati ya Korea na Afrika na pia atakutana na Watanzania waishio Ughaibuni.

A handwritten signature in blue ink, appearing to read 'Zuhura Yunus'.

Zuhura Yunus
Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu

